Rambirambi Za Daktari David Owino

BW. WILSON Agutu wa Mombasa ametoa rambirambi zake kwa kifo cha Dkt. Augostino David Owino aliyeaga dunia Desemba 5 na kuzikwa katika Alego wilayani Siaya Jumanne.

Bw. Agutu amesema katika taarifa yake ya rambirambi kwamba Dkt. Owino ambaye aliaga dunia katika hospitali ya Aga Khan Mombasa, alikuwa daktari aliyejitolea kuwahudumia wagonjwa wake kwa unyenyekevu.

WATENGENEZAJI viatu maridadi za kila aina, Farucci wamekisaidia klabu cha Kiziwi leopards FC flana zitakazowasaidia wachezaji kwa mazoezi. Pichani anaonekana Bw. Hanif Kherdin (kulia) akimkabidhi timu meneja wa Kiziwi, Bw. Ali Ringi.

Asemavyo Mhariri:

MZEE KENYATTA ALITUKOMBOA NA MOI AZIDI KULIIMARISHA TAIFA

• MZEE KENYATTA

MOMBASA ni mmojawapo ya miji ambayo ilijitokeza kwa sura mpya wakati huu ambapo nchi yetu inasherehekea sikuku ya kuadhimisha miaka 20 toka nchi yetu ijinyakulie Uhuru wake na hadi leo, mapambo hayo yanaonekana kwenye barabara kubwa za mji wetu huu wa Mombasa ambao unajulikana kama mji wa pili mkubwa katika Kenya.

WAKENYA wote popote walipo hapa nchini na nye nchi hii wamekuwa katika maandalizi makubwa ya kusherehekea sikukuu hii ya taifa, sikukuu ambayo inatukumbusha siku ambayo bendera ya mbeberu iliteremshwa na tukaipandisha yetu.

MBALI na tamasha na shamrashamra mbali mbali zilizofanyika kote nchini kwa ajili ya sherehe ya siku hii tukufu kwa taifa letu, barabara zetu zilionekana za kupendeza kutokana na mapambo ya kuvutia hasa kwenye barabara zilizo kubwa kama Digo Road, Moi Avenue na Kenyatta Avenue.

MAPAMBO yote haya yalikuwa ya kuadhimisha miaka 20 ya Uhuru wetu na yanakumbusha toka mwaka 1963 ambapo Mtukufu Rais wa Kwanza na Baba wa Taifa, **Hayati Mzee Jomo Kenyatta** alipofanikiwa kututoa katika minyonyoro ya wakoloni. Mzee Jomo Kenyatta ndiye aliyekuwa mwanzilishi wa taifa hili.

WAKATI huu ambapo tunasherehekea miaka 20 ya Uhuru wetu, Baba wa Taifa, **Rais Daniel arap Moi** ndiye anayeshikilia hatamu za kuliongoza taifa letu na yeye anayafuata kwa dhati maongozi ya mwanzilishi wetu, Hayati Mzee Kenyatta na amezidi kulistawisha taifa hili.

HAKIKA tulistahili kusherehekea Uhuru wetu kwa kila aina ya tamasha na tafrija na pia kuipamba miji yetu ili wale wakoloni waliokuwa wakitutawala waone vile hatua kubwa tuliyopiga toka tujinyakulie Uhuru kutoka kwao, hatua ambayo ni wazi ni ya maendeleo ya kudumu.

• RAIS MOI

Clement Gachanja ataka Ripoti

NA ABDULRAHMAN SHERIFF

MWENYEKITI wa shirikisho la Soka nchini (Kenya Football Federation), Bw. Clement Gachanja ameiomba Kamati inayosimamia shughuli za utiaji wa taa (floodlights') katika uwanja wa Manispaa ya Mombasa itume ripoti kamili juu ya maendeleo ya jambo hilo kwa shirkisho lake ili kutafutwe ufumbuzi na ukamilishi wa mpango huo. Bw. Gachanja alitoa ombi hilo wakati alipokutana na wanakamati wa Mombasa Stadium Floodlights Committee katika afisi ya Benham iliyoko mtaa wa Nkrumah mjini Mombasa wiki iliyopita.

Katika mazungumzo yaliyochukua muda mfupi, Bw. Gachanja alisema umefika wakati kwa wananchi ambao wengi wao wamejishirikisha katika kuchangia mpango huo wa taa za stadium ya Mombasa waambiwe kinaganaga juu ya pesa ngapi zimepatikana, ngapi zimeshatumika na ngapi zinatakikana ilia kukamilisha mpango huo.

Mwenyekiti huyo ambaye pia ni Mbunge wa Dagoretti katika mkoa wa Nariobi alisema Mombasa na mkoa wa Pwani ambao kuna chipukizi wanaoweza kuwa wachezaji hodari siku zijazo, wanakosa nafasi ya kujiendeleza kutokana na kutoona mechi nyingi za kimataifa na kukosa nafasi ya kushuhudia kabumbu la hali ya juu.

"Hii inatokana na K.F.F. kuogopa kupeleka mechi nyingi kwenye stadium ya Mombasa kutokana na ukosefu wa taa kwani tunaogopa zisije mechi nyingine zikimalizika na giza kujitokeza wakati mchezo unahitajika kuongezwa wakati", akaongeza Bw. Gachanja.

Bw. Gachanja aliiambia Kamati hiyo kuwa K.F.F. itafanya taratibu za kutayarisha michuano kadha ya kimataifa ili fedha zitakazopatikana zisaidididie mpango huo wa kutiwa taa kwenye uwanja huo. "Tunangojea ripoti yenu ambayo itakuwa na uthibitisho wa fedha zilizotumika ili jambo hili liharakishwe na mashabiki wa Pwani wapate kujionea mechi za maana", akasema.

Bw. Gachanja alimwambia Katibu wa kamati hiyo, Bw. Ben Munyeki kwamba wananchi wamekuwa wakisaidia kuchagisha mpango huo toka 1978 kwa kulipa Shs. 1/- kwa kila mechi iliyochezwa katika stadium hiyo. "Wananchi wanataka kujua ni pesa ngapi zimetumika na zilizopatikana toka walipoanza mchago huo", akaeleza mwenyekiti huyo.

HARAMBEE

Akijibu, Bw. Munyeki ambaye pia ni naibu mkurugenzi wa idara ya huduma za jamii katika Manispaa ya Mombasa alisema Kamati yeke ambayo ni Kama kamati nyingine za Harambee isihusishwe na Manispaa na akaahidi itatayarisha ripoti na kuiwasilisha kwa K.F.F. kwa kipindi cha wiki mbili zijazo.

Alimsifu Bw. Gachanja kwa kuonyesha kuwa na nia ya mpango huo utiliwe mkazo ili

• BW. GACHANJA

ukamilike na akamuomba mwenyekiti huyo kutumia uwezo pia kama kiongozi

Wengine waliokuwako katika mkutano huo ni pamoja na Injinia wa mpango huo. Bw. Charles; mweka hazina wa K.F.F. Bw. C. Mogaka; Katibu mdogo. Bw. Victor Mbaji. Mwenyekiti wa K.F.F. Pwani. Bw. Sadla Khamis na viongozi wengine wa K.F.F. Pwani.

MBINU

katika nchi kutafuta mbinu za jambo hili kukamilika haraka iwezekanavyo.

Alifahamisha kuwa jumla ya karibu 1,000,000/- bado zinahitajika ili mpango huo upate kukamilika. Mpango huo utagharimu karibu 2,500,000/-

Huyu ni Mtumbuizaji wa Mashabiki wa Disco, D. J. Mohammed Sheikh Ali anayejulikana kama "Kenny Disco Master".

KENYA CHARITY SWEEPSTAKE INAWALETEA SHINDANO MAALUM LA KRISMASI HAPO TAREHE 20 DISEMBA.

. ZAWADI YA KWANZA SHS. 10,000/- PAMOJA NA ZAWADI 10 ZA SHS. 1,000/- KILA MOJA NA ZAWADI ZINGINE 10 ZA SHS. 500/- KILA MOJA.

KILA MOJA.

TIKETI HIZO HIZO PIA ZITAJISHINDIA ZAWADI NYINGINE PAMOJA SHS. 200,000/- KATIKA SHINDANO KUBWA LA KILA MWEZI.

JINUNULIE TIKETI ZAKO KABLA YA TAREHE 20 DISEMBA.

MFANYA KAZI HODARI

BI. PAULINE Robert Kilimali aneyetoka Tsunza wilayani Kwale anefanza kazi ya kukusanya kodi za viwanja ya Ali Bin Soud vilivyoko huko shule ya Bomu mjini Mombasa. Bi. Pauline alye

Mombasa. Bi. Pauline aliye na umri wa miaka 21 ni Maonaji Maarufu wa gazeti hili la COASTWEEK kila siku ya Ijuma.

Farucci Coastweek

JISHINDIE VIATU MARIDADI VYA FARUCCI KWA MSHINDI WA KWANZA NA T-SHIRT KWA WASHINDI WA PILI NA WATATU KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO

SWAHILI CROSSWORD No. 176

KWENDA KULIA:

1. Chombo cha kusikizia habari na kuona picha (TV)
6. Mtu asiyejalitaabu, mkaidi asiyekanyika, sugu.
7. Rai, shauri.
8. Unachokimiliki kama pesa, shamba n.k.
10. Salama
13. Sikukuu ya kiislamu.
15. Chumba cha kupumzikia.
16. Zawadi, hidaya.
17. Watayarishe chakula.

KWENDA CHINI:

1. Kula kwa ulimi.
2. .....ikivuma sana hupasuka
3. Ulimi zaidi ya mmoja
4. Itamu Mno.
5. Cha mlango.
9. Ruhusa.
11. Mnyama maridadi mfano wa kima.
12. Ndege.
14. Chanda chema huvishwa.....

Wshindi wa Fumbo La Kujaza maneno No. 175.

1. Mwanaharusi Idd, Sanduku La Posta 8, UKUNDA.

2. Christopher Okollo, Sanduku La Posta 95636, Nyali MOMBASA

3. KATAMBAY WABIAYI Sanduku La Posta 95636, Nyali MOMBASA.

Washindi waombwa wafike afisini mwa COASTWEEK.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANANO No. 175.

KWENDA KULIA

1. BUSTANI, 5. UN, 6. NYEMBAMBA, 7. UNGUJA, 8. BA, 10. UK, 12. JIBWA, 14. UPARA, 15. UA, 16. OA, 17. ALA.

KWENDA CHINI

1. BUNGUU, 2. TUMBUU, 3. NGAMANI, 4. UNA, 5. UBWABWA, 9. AA, 10. UPO, 11. KAA, 12. JAA, 13. BUA.

JINA. ....

SANDUKU LA POSTA. ....

....

Shindano la Fumbo La kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata viatu na T-Shirt maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK limited Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri COASTWEEK, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya jumatano tarehe **Dec. 28, 1983.** Saa nne asubihi shindano hili litakuwa mwisho.